

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**SHULE YA SEKONDARI RUTAMBA**

**S.L.B 439-RUTAMBA LINDI**

MZAZI/MLEZI WA: .....

S.L.B 439

RUTAMBA

LINDI

Ndugu,

**YAH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

Napendakukujulishakuwamwanaonimiongonimwawanafunziwaliochaguliwakujungakatikashule yasekondari rutambakidato cha kwanza 2021.

ShuleyetuitafunguliwasikuyaJumatatutarehe11/01/2021 na mwanao anatakiwa kuripoti shuleni bila kukosa

Mwanaoanatakiwa awe navituvifuatavyo:

**1. SARE ZA SHUIE**

- a) Sale ya shule hii ni mashati (2)meupe na suruali mbili (2)za rangi ya damu ya mzee kwa wavulana. Blauzi mbili (2) nyeupe na sketi mbili (2) za damu ya mzee kwa wasichana.
- b) Mishono ya suruali kwa wavulana.suruali lazima iwe pana na isiwe ya kupana(mdomo).ikiwa modo suruali hiyo itachanwa.
- c) Mishono ya sketi zisiwe zenye malinda mengi.
- d) Tai kwa wavulana na wasichana wasiovaa hijabu na lazima ifanane na rangi ya suruali na sikte.
- e) Kwa wale watakao vaa hijabu rangi ya hijabu ni nyeupe . Urefu ufiki kiunoni.
- f) Sweta rangi ya damu yam zee yenye mshono wa V shingon.
- g) Bukta mbili za rangi nyekundu na flana (T-shirt) mbili rangi ya bluu kwa wavulana. Na track suti mbili rangi ya bluu na Flana mbili (T-shirt za rangi ya bluu. Kwa ajiri ya michezo.

### 3. Maitaji mengine:

- a) Madaftari makubwa (counter book) tisa (9), kalamu na mkebe wa hesabati.
- b) Ndoo moja na jembe kwa ajiri ya usafi.

### 4. Sheria na kanuni muhimu za shule.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na:25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na:10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na offisi ya Raisi (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- i. Heshima kwa viongozi, Walimu, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- ii. Maudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- iv. Kuwai katika kila shughuli za shule na nyengine utakazopewa.
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hyii.
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- viii. Kuzingatiaratiba ya shule wakati wote na
- ix. Kutunza mali za shule.

### 5. makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shulke:

- a) Wizi
- b) Uasharati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevina matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- f) Kudharau bendera ya Taifa
- g) Kupigana au kupiga.
- h) Kuwa mja mzito/ kupata mimba.
- i) Kuoja kuolewa.
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

### 6. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

- a) Medicial Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**NB:**

**Tafadhali soma kwa makini/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARY  
RUTAMBA**

.....

**GEORGE FIGUDA  
MKUU WA SHULE**